# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA 2014/15

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2014

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA
# 2014/15

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2014

## Utangulizi

Tamko la Sera ya Fedha hutolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa sheria ili kuweka bayana malengo ya Sera ya Fedha, msingi wa malengo hayo na hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa kufikia malengo hayo. Tamko hili kwa mwaka 2014/15 linajumuisha mapitio ya utekelezaji wa Sera ya Fedha ya mwaka 2013/14 na kuainisha malengo ya Sera ya Fedha kwa mwaka 2014/15.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Katika kipindi cha mwaka 2013, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2012. Uchumi wa nchi zilizoendelea ulionyesha dalili za kuimarika, wakati nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea uchumi wake ulikua kwa kasi ndogo. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Aprili 2014 (International Monetary Fund (IMF) World Economic Outlook, April 2014), uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2014 na asilimia 3.9 mwaka 2015, kutokana na kulegeza sera ya matumizi ya serikali *(lesser fiscal tightening)* na kuimarika kwa hali ya ukwasi kwenye uchumi.

Katika mwezi Aprili 2014, kasi ya mfumuko wa bei iliongezeka kwenye nchi zilizoendelea na kupungua katika nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi. Kasi ya mfumuko wa bei iliongezeka kwenye mataifa ya Ulaya hasa kutokana na kuongezeka kwa bei za tumbaku na umeme, wakati nchini Marekani ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana na kupanda kwa bei za vyakula na nishati hususan gesi asilia, umeme na mafuta. Nchini Uingereza, kasi ya upandaji bei iliongezeka kutokana na kupanda kwa gharama za usafirishaji, hasa nauli za ndege na mafuta. Hata hivyo, kasi ya upandaji bei ilipungua nchini China kutokana na kupungua kwa bei za vyakula; wakati kule India, kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei kulichangiwa na kushuka kwa bei za madini, mafuta na nishati.

Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Aprili 2014, inaonyesha matarajio ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei hadi wastani wa asilimia 1.5 mwaka 2014, kutoka asilimia 1.4 mwaka 2013 katika nchi zilizoendelea. Hata

hivyo, mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2014, kutoka asilimia 6.2 mwaka 2013 katika nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kiuchumi kutokana na kushuka kwa mahitaji na bei za bidhaa.

**Mwenendo wa Uchumi Tanzania**

***Tanzania Bara***

Katika mwaka 2013, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 kwa mwaka 2012. Ukuaji huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji kwenye sekta za mawasiliano, huduma za kifedha, ujenzi, biashara za jumla na rejareja pamoja na viwanda. Katika mwaka 2014/15, Pato la Taifa linatarajiwa kuendelea kukua kwa zaidi ya asilimia 7. Hali hii itatokana na uwekezaji unaoendelea katika sekta ya miundombinu hasa barabara, reli na nishati. Ukuaji wa Pato la Taifa unatarajiwa pia kuchangiwa na hali nzuri ya hewa, kuimarika kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, pamoja na kuimarika kwa uchumi wa dunia utakaoongeza mapato yetu katika mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

Mfumuko wa bei ulibakia katika kiwango cha tarakimu moja katika miezi 10 ya mwanzo ya mwaka 2013/14. Hali hii ilitokana na sera madhubuti ya fedha, kuimarika kwa hali ya chakula, pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia. Kasi ya mfumuko wa jumla wa bei *(headline inflation)* ilipungua hadi asilimia 6.3 Aprili 2014, kutoka asilimia 7.5 mwezi Julai 2013, wakati kasi ya mfumuko wa bei za vyakula *(food inflation)* ilipungua kufikia asilimia 7.8 kutoka asilimia 8.0. Wakati huo huo, kasi ya mfumuko usiojumuisha bei za vyakula na nishati *(core inflation)* ilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.3, kutoka asilimia 6.7. Katika mwaka wa fedha 2014/15, mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia kwenye kiwango cha tarakimu moja, ingawa changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu wa chakula katika ukanda wa Afrika Mashariki na kutokutabirika kwa hali ya kisiasa katika nchi za Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika zinaweza kusababisha ongezeko la bei za chakula na mafuta.

Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014, mapato taslimu ya Serikali *(on cash basis)* yalifikia asilimia 88.0 ya malengo ya kipindi hicho. Upungufu katika

mapato ya ndani ulichangiwa na kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya hatua za kuongeza mapato katika bajeti ya 2013/14. Matumizi ya Serikali *(on cash basis)* yalikuwa asilimia 72.0 ya makadirio ya kipindi hicho, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa asilimia 92.0 ya makadirio. Matumizi ya maendeleo yalikuwa asilimia 37.9 tu ya makadirio kutokana na baadhi ya wahisani kuchelewa kutoa fedha za miradi ya maendeleo pamoja na kutokupatikana kwa fedha za mikopo ya kibiashara *(external non-concessional loans)*.

Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali na nchi za nje *(current account deficit)* iliongezeka na kufikia dola za Kimarekani milioni 3,857.5 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 3,371.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2012/13. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za walaji kutoka nje hususan madawa, bidhaa za karatasi na plastiki, pamoja na kiwango kikubwa cha uagizaji wa mafuta. Hadi mwezi Aprili 2014, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani milioni 4,647.5 ambayo ingetosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa wastani wa kipindi cha miezi 4.6. Kiasi hicho hakijumuishi bidhaa na huduma zinazolipiwa kutokana na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Katika kipindi hicho, akiba ya rasilimali za fedha za kigeni katika mabenki ilikuwa dola za Kimarekani milioni 845.4.

Deni la nje liliongezeka kwa asilimia 19.7 na kufikia dola za Kimarekani milioni 13,938.1 mwishoni mwa mwezi Aprili 2014, ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 11,647.4 kilichofikiwa mwezi Aprili 2013. Uwiano wa deni la nje kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 41.9 mwishoni mwa Aprili 2014; kati ya kiasi hicho uwiano wa deni la umma kwa Pato la Taifa ulikuwa asimilia 35.3. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la taifa *(Debt Sustainability Analysis)* iliyofanyika kwa kutumia takwimu za mwezi Juni 2013, yanaonyesha kuwa thamani ya sasa ya deni la nje ni sawa na asilimia 19.5 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na kiwango cha kimataifa cha asilimia 50. Hali hii inaonyesha kwamba deni la nje bado ni himilivu. Wakati huo huo, deni la ndani la umma liliongezeka kwa asilimia 19.3 hadi kufikia Shilingi bilioni 6,542.0.

Takwimu za tathmini ya hali ya mabenki zinaonyesha kuwa sekta ya mabenki imeendelea kuwa imara na salama, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Sekta hii imeendelea kupata faida kabla ya kodi ambayo imeongezeka kwa asilimia 3.1 kutokana na juhudi za mabenki kukusanya mikopo iliyokuwa imefutwa *(written-off loans)*. Usimamizi wa biashara zinazohusiana na shughuli za kibenki na utimizaji wa masharti ya kuzuia utakatishaji wa fedha haramu umeimarishwa. Mfumo wa kulinda wateja wanaotumia huduma za kifedha *(Consumer Protection Framework)* unaandaliwa. Aidha, Benki Kuu iko katika hatua za mwisho za kurekebisha kanuni za kusimamia mabenki (Prudential Regulations for Banking Institutions) ili kukidhi mabadiliko katika huduma za kibenki yaliyotokea hivi karibuni kwenye sekta hiyo. Kanuni hizi zinatarajiwa kutangazwa katika gazeti la serikali mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2014/15.

Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wasiofikiwa na huduma za kibenki umeongezeka kutokana na ubunifu wa mipango ya utoaji wa huduma za malipo ya reja reja kupitia simu za mikononi. Ubunifu huu umeongeza idadi ya watu wanaopata huduma za kibenki maradufu kwa kipindi cha miaka minne tangu mwaka 2009. Aidha, huduma za uwakala wa mabenki *(agent banking services)* zimeendelea kukua. Hadi Aprili 2014, benki tano zilikuwa zikitoa huduma hizo, na idadi ya mawakala iliongezeka na kufikia 840 kutoka 304 mwezi Septemba 2013, wakati huduma hizo zilipoanzishwa. Kuanzishwa hivi karibuni kwa M-Pawa kunatoa fursa kwa huduma za kibenki za kuweka amana na kukopa kupitia simu za mikononi, na hivyo kufanya huduma za kibenki ziwafikie watu wengi zaidi.

Mifumo ya Taifa ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ubora ikiwa ni pamoja na mfumo wa malipo baina ya mabenki *(Tanzania Inter-Bank settlement System – TISS)* kuanza kutumika hata siku za Jumamosi kuanzia Desemba 2013. Utaratibu huu una lengo la kukuza uwezo wa serikali kukusanya mapato na kupunguza ulimbikizaji wa kodi unaofanywa na mabenki. Aidha, hazina ndogo zilizopo katika mikoa na manispaa zimeanza kufanya malipo kupitia TISS na hivyo kuharakisha malipo na kupunguza udanganyifu unaotokana na kutumia hawala za fedha. Tanzania ilijiunga na Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki *(East Africa Payments System - EAPS)* tangu mfumo huu ulipoanzishwa mwezi Novemba

2013. Mfumo huu unawezesha malipo ya papo kwa papo kwa kutumia sarafu za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mfumo huu unarahisisha biashara, malipo, na uwekezaji katika kanda ya Afrika Mashariki.

***Zanzibar***

Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.4 mwaka 2013, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.1 wa mwaka 2012. Ukuaji huu ulichochewa kwa kiasi kikubwa na ukuaji kwenye sekta za utalii, kilimo, mawasiliano, ujenzi, huduma za kifedha na biashara.

Mfumuko wa jumla wa bei ulikuwa asilimia 5.3 mwezi Aprili 2014, ikilinganishwa na asilimia 3.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana hasa na ongezeko la bei za mchele, ndizi na mkaa. Hata hivyo, kiwango hiki cha mfumuko wa bei ni mojawapo ya viwango vya chini zaidi katika kanda ya Afrika Mashariki.

Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014, mapato ya ndani yalitosha kugharamia matumizi ya kawaida ya Serikali. Mapato ya Serikali yalikuwa asilimia 99.7 ya lengo katika kipindi hicho. Matumizi ya Serikali yalikuwa juu ya makadirio kwa asilimia 2.8. Wakati huo huo, nakisi katika bajeti ya serikali ilikuwa shilingi bilioni 59.0 ambayo iligharamiwa na mikopo kutoka nje kwa asilimia 83.1, na kiasi kilichobakia kilitokana na vyanzo vya ndani.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali ilipungua hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 9.8 kutoka dola za Kimarekani milioni 34.5 katika kipindi cha Julai 2012 hadi Aprili 2013. Hali hii ilisababishwa na kupungua kwa malipo ya huduma za afya, elimu, na shughuli binafsi nje ya nchi.

**Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2013/14**

***Malengo ya Sera ya Fedha***

Katika mwaka wa fedha 2013/14, Benki Kuu ya Tanzania iliweka malengo yafuatayo ili kuyafikia malengo ya uchumi mpana ya Serikali kwa kuweka ukwasi unaowiana na mahitaji ya uchumi:

i. Ukuaji wa wastani wa `fedha taslimu usiozidi asilimia 14.0;
ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 15.0;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 19.6 unaowiana na malengo ya ukuaji wa ujazi wa fedha; na
iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa zinazogharamiwa na wawekezaji kutoka nje ya nchi *(Foreign Direct Investment)* kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha***

Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014, ukuaji wa ujazi wa fedha na karadha ulikuwa ndani ya malengo. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15 ifikapo Juni 2014. Wakati huo huo, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 16 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 19.6.

Katika kipindi hicho, ukwasi katika mabenki ulikuwa wa kuridhisha kama ilivyojionyesha katika mwenendo wa riba katika soko la fedha. Riba za dhamana za serikali zilipungua, wakati zile za soko la kukopeshana baina ya mabenki hazikubadilika sana. Wakati huo huo, wastani wa fedha taslimu *(average reserve money)* uliendelea kubaki ndani ya malengo isipokuwa mwezi Desemba 2013 ambapo lengo lilivukwa kwa Shilingi bilioni 5.8 tu. Aidha, thamani ya shilingi kwa Dola ya Kimarekani ilipungua kwa asilimia 2.2 na kufikia wastani wa Shilingi 1,612 kwa Dola. Kasi ya kushuka kwa thamani ya Shilingi iliongezeka

hivi karibuni kutokana na ongezeko la uagizaji wa mafuta kutoka nje na kushuka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa nje. Hali hii inatarajiwa kutengemaa katikati ya mwezi Juni 2014 kufuatia kuanza kwa msimu wa mauzo ya mazao asilia nje ya nchi na kuanza kwa msimu wa utalii.

**Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2014/15**

Katika mwaka wa fedha 2014/15, Sera ya Bajeti itajikita katika kuendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, MKUKUTA II na MKUZA II hususan programu za kipaumbele zilizoanishwa kwenye kauli mbiu ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN) kwa kuzingatia kiwango cha nakisi ya bajeti kilichowekwa. Kuimarishwa kwa sera za ukusanyaji na usimamizi wa kodi, matumizi na madeni ya Serikali, kutachangia kufikiwa kwa malengo hayo. Uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 7.3 mwaka 2014/15 kwa kutumia vigezo vya matarajio ya ukuaji wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2014 na asilimia 7.4 mwaka 2015, na kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki katika tarakimu moja.

Ili kuyafikia malengo ya sera za uchumi, Sera ya Fedha itajikita katika kufikia malengo yafuatayo, ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa huduma za kibenki kwa wananchi wasiofikiwa na huduma hizo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 14.0;
ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 15.5;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 16.0 unaowiana na malengo ya ukuaji wa ujazi wa fedha; na
iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa zinazogharamiwa na wawekezaji kutoka nje ya nchi *(Foreign Direct Investment)* kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Muundo na utekelezaji wa Sera ya Fedha utaendelea kuzingatia mfumo wa kudhibiti ukuaji wa fedha taslimu ukitumia nyenzo mbalimbali za Sera ya Fedha zitakazohakikisha kuwa ukwasi unabakia ndani ya malengo. Juhudi zinafanywa

kuimarisha soko la fedha ili kuongeza ufanisi katika Sera ya Fedha ikiwa ni hatua ya awali katika kujiandaa kutumia riba ya Benki Kuu *(policy rate)* kama kiashiria cha mwelekeo wa Sera ya Fedha.

Soko la dhamana za Serikali litaendelea kutoa mwelekeo wa riba katika soko la fedha. Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa ufanisi katika soko la fedha kwa kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo uwazi zaidi ili kupunguza mabadiliko makubwa ya riba za dhamana za serikali.

Kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni kati ya mabenki katika soko la jumla *(Inter-bank Foreign Exchange Market)* kitaendelea kuongozwa na nguvu za soko. Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la fedha za kigeni kwa ajili ya kuhakikisha kiwango cha ujazi wa fedha kinakuwa ndani ya malengo na kupunguza madhara ya mabadiliko makubwa na ya ghafla katika kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni. Haya yote yatatekelezwa kwa kuzingatia malengo ya akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, pamoja na hatua za hivi karibuni za Tanzania kuruhusu uwekezaji wa mitaji bila vikwazo miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyokubaliwa kwenye Itifaki ya Soko la Pamoja. Benki Kuu imetayarisha miongozo na kanuni zitakazosimamia utekelezaji wa ushiriki wa nchi wanachama wa Afrika Mashariki katika uwekezaji.

**Hitimisho**

Mkakati wa Benki Kuu kudhibiti ujazi wa fedha katika mwaka wa fedha 2013/14 umesaidia kudhibiti mfumuko wa bei na kuleta uimara wa viwango vya ubadilishanaji wa fedha za kigeni. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Benki Kuu itaendelea kuwa makini kuchukua hatua sahihi dhidi ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na upungufu wa chakula katika kanda ya Afrika Mashariki pamoja na mwenendo wa uchumi wa dunia ambao unaweza kuongeza kasi ya mfumuko wa bei.

Kutokana na juhudi za serikali za kuboresha miundombinu ikiwemo barabara, reli na uwekezaji kwenye nishati, uchumi unatarajiwa kukua kwa zaidi ya asilimia 7 katika mwaka 2014/15. Ukuaji huu pia utachochewa na kuimarika kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, hali nzuri ya hewa pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, kutokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia.

Katika mwaka 2014/15, Benki Kuu itaendelea kuongeza ufanisi katika soko la fedha kwa kuongeza uwazi katika matumizi ya nyenzo mbalimbali za utekelezaji wa Sera ya Fedha ikiwa ni hatua ya awali katika kujiandaa kutumia riba ya Benki Kuu *(policy rate)* kama kiashiria cha mwelekeo wa Sera ya Fedha. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua sahihi ili kuhakikisha huduma za kifedha zinawafikia wananchi wengi zaidi huku ikizingatia utulivu katika sekta ya fedha. Kwa kuendeleza ushirikiano katika kutekeleza Sera za Bajeti na Fedha, Benki Kuu inaamini kwamba malengo ya Sera ya Fedha kwa mwaka 2014/15 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo 11884, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328/9, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Printed by Identity Promotion Ltd